# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.12 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) FEBRUARI 2022

## WAZIRI BASHUNGWA AWAAGIZA WAKUU WOTE WA MIKOA NCHINI KUMPA TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 15,000 YA MAMA SAMIA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (kwenye mimbari), akiwasilisha hotuba yake kwa Menejimenti na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu – TSC (hawapo pichani), alipokuwa akifanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

## KARIBU WAZIRI BASHUNGWA, TUNAKUAHIDI USHIRIKIANO ULIOTUKUKA KATIKA KULETA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU NCHINI

Siku za hivi karibuni, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, Mwalimu Paulina Nkwama, kwa niaba ya Uongozi na Wafanyakazi wote wa TSC wakati akiwasilisha maelezo ya awali ya ufunguzi wa mkutano wa baraza la wafanyakazi aliahidi kwa Waziri wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa, kutoa ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha Utumishi wa Walimu unasimamiwa ipasavyo ili kupunguza malalamiko na kero za walimu na wadau wanaohudumiwa na Tume ili hatimaye kuinua kiwango cha elimu hapa nchini.

Pamoja na mambo mengine muhimu; aliipongeza Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ubunifu mkubwa wa kutengeneza na kuzindua Mwongozo wa Kalenda ya Utekelezaji wa Mitaala iliyozinduliwa Januari 14, 2022 huku akimhakikishia Waziri Bashungwa, kuwa TSC itakuwa bega kwa bega katika kuhimiza matumizi ya Kalenda hiyo kama nyezo muhimu kwa kuhakikisha kuwa kila shule inazingatia na kufikia malengo yanayotarajiwa.

Ni wazi kuwa utekelezaji wa mitaala utasaidia kwa kiwango kikubwa kuimarisha na kuboresha zaidi utoaji wa elimu. Katika kuboresha zaidi utekelezaji huo aliendelea kuwakumbusha walimu wote nchini kuzingatia Maadili ya Kazi ya Ualimu, hasa; wajibu wao kwa mtoto kumlea kimwili, kiakili, kijamii na kiroho, wajibu kwa Mwajiri, kazi yao ya ualimu, Jamii, na Taifa kwa ujumla wake.

Haya yote yanapaswa kulandana na jitihada za Mhe. Rais kwani katika kipindi kifupi Serikali imeweza kujenga madarasa 15,000 yakiwemo madarasa 12,000 ya Shule za Sekondari na Madarasa 3,000 kwa ajili ya vituo shikizi vya Shule za Msingi. Ujenzi huu umesaidia kuondoa changamoto ya upungufu wa madarasa kwa wanafunzi wanaojiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza na Darasa la Kwanza mwezi Januari, 2022.

Hivi karibuni Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kupatikana kwa fedha za jumla ya shilingi trilioni 1.3 na kuelekeza katika kuboresha miundombinu ya sekta mbalimbali ikiwemo Elimu katika kupambana na UVIKO-19.

TSC tunasema; walimu ni nguzo muhimu sana katika Taifa lolote duniani ili kupambana kiuhalisia na maadui wakubwa wa maendeleo ya nchi; Ujinga, Maradhi, na Umaskini. Hivyo, tunapongeza uimarishaji wa miundombinu yao.

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

**KATUNI**




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# WAZIRI BASHUNGWA AWAAGIZA WAKUU WOTE WA MIKOA NCHINI KUMPA TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 15,000 YA MAMA SAMIA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (kwenye mimbari), akiwasilisha hotuba yake kwa Menejimenti na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu – TSC (hawapo pichani), alipokuwa akifanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa, amewaagiza Wakuu wote wa Mikoa nchini, kuwasilisha taarifa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 15,000, vinavyotambulika na wananchi kama 'Madarasa ya Mama Samia' kabla au ifikapo Januari 25, mwaka huu.

Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 15,000 yakiwemo madarasa 12,000 ya Shule za Sekondari na madarasa 3,000 kwa ajili ya vituo shikizi vya Shule za Msingi nchini kote ili kuondoa changamoto ya upungufu wa madarasa kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza..

Bashungwa ametoa agizo hilo hivi karibuni wakati alipokuwa akifanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza za Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC), uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma.

Alisema Wakuu wa Mikoa, wanatakiwa kujiridhisha na taarifa hizo kabla ya kuziwasilisha kwa kuzingatia taratibu na miongozo waliyopewa kama imefuatwa ili kuona kama pesa iliyotolewa inaendana na thamani halisi ya ujenzi wa madarasa hayo.



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), pamoja na meza kuu; Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa tatu kulia), Katibu Mkuu (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (wa pili kushoto), Naibu Katibu Mkuu – Elimu (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (wa kwanza kushoto), na Katibu wa TSC na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kulia), na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi TSC Ndg. Laurence Chankan (wa kwanza kulia) mara baada ya Waziri kuwasili.*

# WAZIRI BASHUNGWA AWAAGIZA WAKUU WOTE WA MIKOA NCHINI KUMPA TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 15,000 YA MAMA SAMIA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19



*Sehemu ya wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakifuatilia mjadala katika mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*

"Nitumie fursa hii kuwaeleza Wakuu wa Mikoa, kuwasilisha taarifa za ujenzi kabla ya Januari 25, mwaka huu, ila kwanza wajiridhishe na taarifa hizo kama thamani ya fedha katika ujenzi huo imepatikana," alisema.

Aidha Bashungwa ameitaka TSC kuweka dawati maalum la kuwahudumia wastaafu ambalo litasaidia kufuatilia haki zao pindi watakapokuwa wakifuatilia haki zao za msingi baada ya utumishi wao kukoma kwa mujibu wa Sheria huku akiahidi kushughulikia changamoto zote za Tume ili kuiboresha ifanye kazi vizuri na kwa ufanisi zaidi.

"Wekeni dawati kwa ajili ya kuwahudumia wastaafu wanaofuatilia haki zao ili kama wakizungushwa sehemu husika basi walau waweze kufika na kusikilizwa au wapate hata fursa ya kupiga simu, ni vizuri Tume iwe sehemu ya faraja kwao," alisema.

Kwa upande mwingine, Waziri Bashungwa ameonesha matumaini kwa Tume hiyo na kuitaka kuendelea kufanya kazi kwa weledi na mshikamano ili kuwa na walimu bora watakaoinua kiwango cha elimu nchini.

Alisema nchi inahitaji kuwa na walimu wazalendo, wawajibikaji na wanaotambua maadili ya kazi zao na siyo bora walimu.

"Mmefafanua namna mlivyojipanga kuunga mkono jitihada za Rais wetu mpendwa katika kuboresha elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunakuwa na walimu ambao ni bora na siyo bora walimu," alisema Waziri Bashungwa.

Mheshimiwa Bashungwa alisema Tume ina wajibu wa kuhakikisha walimu wanaopewa fursa ya kufundisha watoto, wanakuwa na nidhamu na maadili mema ya kazi yao huku wakizingatia nguzo kuu za ualimu ili kupata matokeo chanya kwa wanafunzi wanaowalea.

Pia Bashungwa aliipongeza Tume hiyo kwa kutowafumbia macho walimu wasiozingatia maadili ya kazi yao ambapo jumla ya walimu 1,795 walichukuliwa hatua za kinidhamu kwa makosa mbalimbali huku walimu 931 sawa na asilimia 51.9 wakiongoza kwa kosa la utoro kazini.

# MWENYEKITI TSC, PROF. WILLY KOMBA, AMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUJALI SEKTA YA ELIMU HUKU AKITEKELEZA ILANI YA UCHAGUZI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba, amempongeza kwa dhati Mhe. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyojali Sekta ya Elimu huku akitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 kipengele Na.80 inayolenga: "Kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi."

Aliyasema hayo katika Maelezo ya Utangulizi ya Ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo uliofanyika siku chache zilizopita katika Ukumbi wa 'Jakaya Kikwete Convention'



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa pili kushoto), pamoja na Katibu Mkuu (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (wa pili kulia), Naibu Katibu Mkuu – Elimu (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (wa tatu kulia), na Katibu wa TSC na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto), wakimpokea Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), alipowasili kufungua Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa kwanza kulia), Katibu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kulia), Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu (TSC), Ndg. Moses Chitama (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu (TSC), Mwl. Christina Happe (wa kwanza kushoto), na Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi (TSC), Ndg. Neema Lemunge (wa pili kulia), katika tete-a-tete mara baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

# MWENYEKITI TSC, PROF. WILLY KOMBA, AMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUJALI SEKTA YA ELIMU HUKU AKITEKELEZA ILANI YA UCHAGUZI



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), pamoja na meza kuu; Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa tatu kulia), Katibu Mkuu (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (wa tatu kushoto), Naibu Katibu Mkuu – Elimu (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (wa pili kushoto), Katibu wa TSC na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kulia), Katibu wa Baraza la Wafanyakazi TSC Ndg. Laurence Chankan (wa kwanza kulia), na Naibu Katibu Mkuu – TUGHE Taifa Ndg. Rugemalira Rutatina (wa kwanza kushoto), wakiimba wimbo wa mshikamano mara baada ya Waziri kuwasili kwa ufunguzi wa mkutano huo.*

jijini Dodoma.

Hali kadhalika, Prof. Komba, ameipongeza na kuunga mkono dhamira na hatua ya dhati ya Mhe. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kujali Sekta ya Elimu huku akitekeleza Ilani ya CCM Na.80; jambo alilosisitiza linapaswa kuungwa mkono na kila mpenda maendeleo ya Taifa lake kwani ni dhahiri uhaba wa vyumba vya madarasa utabaki kuwa historia baada ya ujenzi wa madarasa 12,000 ya Sekondari na 3,000 ya shule shikizi za msingi hapa nchini yaliyotokana na fedha za kuimarisha mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Sisi (Tume ya Utumishi wa Walimu - TSC) kama wasimamizi wa Utumishi na Maadili ya Walimu, tutahakikisha kuwa tunasimamia ipasavyo masuala ya ajira, nidhamu na maendeleo ya walimu ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na walimu walio bora kwa ajili ya kuwalea Watoto wetu na hatimaye kuinua kiwango cha elimu nchini." Alisema Prof. Komba

Aidha, Mwenyekiti huyo wa TSC, aliipongeza Serikali kwa jitihada zake za kupambana na janga la ugonjwa wa COVID/ UVIKO-19 na kuweka bayana kuwa TSC inaendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Serikali na Wataalamu wa Afya nchini katika kupambana na janga hili huku akiendelea kuwasisitiza na kutilia mkazo kwa watumishi na wadau wa Tume kuchukua tahadhari zote dhidi ya janga hilo katika vikao vyote vya Tume ikiwa ni pamoja na kuchanja. "Rai yangu kwenu ambao hamjachanja, mkachanje."

Vilvile, Prof. Komba, aliwataka walimu wote nchini kushirki kikamilifu katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa kuwa walimu ni sehemu kubwa ya Watumishi wa Umma ambao wanaishi katika mitaa, vijiji na vitongoji; hivyo ni rahisi kuwafikia wananchi na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa Sensa itakayofanyika mwaka 2022.

Nae Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, akitoa maelezo ya utangulizi wakati wa Ufunguzi wa Mkutano huo alisema "Tume inaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi wakiwemo walimu. Katika usimamizi wa Maadili na Nidhamu ya Walimu katika mwaka 2020/2021 Tume imeweza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya walimu 1,795 kwa makosa mbalimbali ambapo kosa la utoro limeongoza kwa kuwa na walimu 931 (51.9%) na asilimia 49.1% ni makosa mengine."

Alisema, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi za Wilaya ziliwezeshwa kufanya ziara shuleni kuwaelimisha walimu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Maadili/ Miiko ya Ualimu, Haki na Wajibu wa Mwalimu.

# WAZIRI BASHUNGWA AIPONGEZA TSC KWA NAMNA INAVYOMUUNGA MKONO MAMA SAMIA KUBORESHA ELIMU NCHINI KWA KUHAKIKISHA NCHI INAKUWA NA WALIMU BORA, WAZALENDO, WAWAJIBIKAJI NA WANAOTAMBUA MAADILI YA KAZI



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai), pamoja na meza kuu; wakielekea eneo la kupiga picha ya pamoja mara baada ya kufanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa, ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa namna ilivyojipanga katika kuunga mkono jitihada za Rais katika kuboresha elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha nchi inakuwa na Walimu ambao ni bora na siyo bora Walimu wenye uzalendo na nchi yao, wawajibikaji na wanaotambua maadili ya kazi yao.

Waziri Bashungwa aliyasema hayo siku za hivi karibuni wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika katika Ukumbu wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

"Naipongeza sana Tume kwa namna ilivyojipanga kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais katika kuboresha elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha nchi inakuwa na Walimu ambao ni bora na siyo bora Walimu, wakiwa wenye uzalendo na nchi yao, wawajibikaji na wanaotambua maadili ya kazi yao." Alisema Waziri Bashungwa

Alisema pamoja na ari ya uboreshaji elimu ya awali,



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), pamoja na meza kuu katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mara baada ya kufanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

# WAZIRI BASHUNGWA AIPONGEZA TSC KWA NAMNA INAVYOMUUNGA MKONO MAMA SAMIA KUBORESHA ELIMU NCHINI KWA KUHAKIKISHA NCHI INAKUWA NA WALIMU BORA, WAZALENDO, WAWAJIBIKAJI NA WANAOTAMBUA MAADILI YA KAZI



*Sehemu ya Menejimenti na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakisali sala ya Tume kabla ya kuanza kwa mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

msingi na sekondari hapa nchini iliyoonyeshwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ina wajibu wa kuhakikisha Walimu wanaopewa fursa ya kufundisha watoto wetu wanakuwa na maadili mema ili kupata matokeo chanya kwa wanafunzi wanaowalea kwani kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeungana na Rais kuwezesha utoaji wa huduma ya elimu kwa wananchi.

"Natambua lengo la Mabaraza ya Wafanyakazi kama hili ni kutafuta ufumbuzi wa kero zenu, lakini pamoja na hilo niwaombe mkaboreshe usimamizi wa utumishi wa Walimu katika masuala yao ya ajira nidhamu na maendeleo yao." Alisema

Pia, Waziri Bashungwa alitoa taarifa kuwa OR- TAMISEMI ina Mfumo wa kupokea malalamiko na kuagiza kwenye Halmashauri zote nchini kubandika kwenye mbao za matangazo namba maalumu ya wananchi na wadau mbalimbali kutuma malalamiko yao pale wanapohitaji kufanya hivyo bila kuwa na kikwazo cha sehemu ya kuwasilisha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa, akihitimisha hotuba yake aliwakumbusha na kuwahimiza wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi na Watumishi wote wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kupata chanjo na kuendelea kuchukua hatua za kujilinda dhidi ya janga la UVIKO-19 lililoikumba nchi yetu tangu mwaka 2019 kwani Serikali kupitia Wizara ya Afya, imefanya jitihada mbalimbali za kuelimisha ikiwa ni pamoja na kuleta chanjo nchini na kuwataka ambao hawajachanjwa kujitokeza kuchanjwa kwa ajili ya kulinda afya na uhai lakini pia kila mmoja katika eneo lake kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo. Alitoa rai hiyo wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC jijini Dodoma Januari 20, 2022.

# OR-TSC NA OR-TAMISEMI ZAJENGA MFUMO WA KIELEKTRONIKI; TEACHERS SERVICE COMMISSION MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM (TSCMIS) KURAHISISHA UTEKELEZAJI MAJUKUMU YA TUME



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama (kwenye mimbari), akitoa maelezo ya utangulizi kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (mwenye suti ya bluu), kwa neno la ukaribisho na kumkaribisha Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai), kwa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

**Na. Mwandishi wetu - Dodoma**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, amesema TSC kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanikiwa kwa hatua za awali kujenga Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama Teachers Service Commission Management Information System (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume huku hatua za ujenzi wa Mfumo huo zikiwa zimekamilika na kufanyiwa majaribio kwa Moduli tatu (3) kati ya sita (6) zilizokusudiwa.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyazi – TSC, Mwl. Paulina Nkwama (aliyesimama), akitoa mwongozo wa mkutano wa baraza uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022. Kushoto kwake aliyekaa ni Katibu wa Baraza hilo Ndg. Lawrence Chankan*

Mwl. Nkwama aliyasema hayo akitoa maelezo ya Utangulizi ya Ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'Jakaya Kikwete Convention' jijini Dodoma hivi karibuni.

"Kwa hatua za awali sisi Tume kwa kushirikiana na TAMISEMI tumefanikiwa kujenga Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama Teachers Service Commission Management Information System (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya TSC huku hatua za ujenzi wa Mfumo huo zikiwa zimekamilika na kufanyiwa majaribio kwa Moduli tatu (3) kati ya sita (6) zilizokusudiwa, hatua za kuwezesha kukamilika kwa moduli zilizosalia zinaendelea. Alisema Mwl. Nkwama

# OR-TSC NA OR-TAMISEMI ZAJENGA MFUMO WA KIELEKTRONIKI; TEACHERS SERVICE COMMISSION MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM (TSCMIS) KURAHISISHA UTEKELEZAJI MAJUKUMU YA TUME



*Sehemu ya wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakifuatilia mjadala katika mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*

Katibu wa Tume na Mwenyekiti huyo wa Baraza aliahidi kwa niaba ya Uongozi na Watumishi wa TSC kutoa ushirikiano wa dhati kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Innocent Bashungwa, katika kuhakikisha Utumishi wa Walimu unasimamiwa ipasavyo ili kupunguza malalamiko na kero za walimu na wadau wanaohudumiwa na Tume ili hatimaye kuinua kiwango cha elimu hapa nchini.

Aidha, Mwl. Nkwama, ameipongeza Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ubunifu mkubwa wa kutengeneza na kuzindua Mwongozo wa Kalenda ya Utekelezaji wa Mitaala iliyozinduliwa Januari 14, 2022 huku akimhakikishia Waziri Bashungwa, kuwa TSC itakuwa bega kwa bega katika kuhimiza matumizi ya Kalenda hiyo kama nyezo muhimu kwa kuhakikisha kuwa kila shule inazingatia na kufikia malengo yanayotarajiwa.

"Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021, pamoja na majukumu mengine TSC iliweza kuwapandisha vyeo walimu wote 126,346 waliokuwa na sifa na kushiriki katika zoezi la kuajiri walimu 14,949." Alisema

Vilevile, Katibu wa huyo wa Tume na Mwenyekiti wa Baraza hilo Mwl. Nkwama, aliendelea kuwakumbusha na kutoa rai kwa walimu wote nchini kuhusu kuzingatia Maadili ya Kazi ya Ualimu, hasa; kuhusu wajibu wao kwa mtoto waliopewa kumlea kimwili, kiakili, kijamii na kiroho, wajibu kwa Mwajiri, kazi yao ya ualimu, Jamii, na Taifa kwa ujumla wake.

Pamoja na hilo alisema Tume inaunga mkono jitihada za Rais katika kuboresha elimu hapa nchini kwa kuzingatia kuwa katika kipindi kifupi Serikali imeweza kujenga madarasa 15,000 yakiwemo madarasa 12,000 ya Shule za Sekondari na Madarasa 3,000 kwa ajili ya vituo shikizi vya Shule za Msingi jambo ambalo limesaidia kuondoa changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa kwa wanafunzi wanaojiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza mwezi Januari, 2022.

Akiwasilisha alisema pamoja na majukumu mengine ya msingi moja ya malengo ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), ni pamoja na kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Umma Tanzania Bara.

"TSC ina majukumu inayoyatekeleza kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwa pamoja na; kutathmini hali ya Walimu na kumshauri Waziri mwenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini; Ajira na Usajili wa Walimu, Kuthibitisha kazini, Kupandisha vyeo, Kubadilishia vyeo Walimu waliojiendeleza kielimu, Kuhakikisha uwiano sawa katika upangaji wa Walimu, Kusimamia Mpango wa Mafunzo wa Walimu, Kutoa Vibali vya kustaafu, kushughulikia Maombi ya kuajiriwa upya, kushughulikia Mafao ya hitimisho la kazi ya Walimu, kushughulikia masuala ya Maadili na Nidhamu za Walimu, Rufaa za Walimu, na ina wajibu wa kumshauri Waziri kuhusu usimamizi na uendelezaji wa Utumishi wa Walimu." Alisema Mwl. Nkwama

# MSIWAFUMBIE MACHO WALIMU WASIOZINGATIA MAADILI YA KAZI YAO NA WACHUKULIWE HATUA ZA KINIDHAMU - WAZIRI BASHUNGWA



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa pili kushoto), pamoja na Katibu Mkuu (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (wa pili kulia), Naibu Katibu Mkuu – Elimu (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli (wa tatu kulia), na Katibu wa TSC na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto), wakimpokea Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), alipowasili kufungua Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa, ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kutowafumbia macho walimu wasiozingatia maadili ya kazi yao kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa makosa mbalimbali.

Alisema jumla ya walimu 1,795 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 huku kosa la utoro kazini likiongoza kwa jumla ya walimu 931 (51.9%) sio idadi ndogo kwani imevuka nusu ya idadi ya mashauri yaliyopokelewa, kufanyiwa uchambuzi, kusikilizwa, na kutolewa uamuzi.

Waziri Bashungwa alitoa pongezi hizo wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'Jakaya Kikwete Convention' jijini Dodoma hivi karibuni.

Hali kadhalika, Waziri Bashungwa alisema anasikitishwa sana na jambo la utoro wa walimu katika vituo vyao vya kazi na kutoa rai kwa Tume kuwa pale inapotokea Mwalimu anakuwa mtoro na kuwanyima wanafunzi haki ya kufundishwa ni wazi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inapaswa kuwachukulia hatua za kinidhamu mara moja walimu kama hao.

Aidha, aliitaka Tume ya



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa, akikabidhi zawadi kama sehemu ya mkono wa pongezi na kheri kwa mmoja wa wastaafu 15 wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nchini aliyestaafu kwa mujibu wa Sheria. Alitoa mkono huo wa pongezi mara baada ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

# MSIWAFUMBIE MACHO WALIMU WASIOZINGATIA MAADILI YA KAZI YAO NA WACHUKULIWE HATUA ZA KINIDHAMU - WAZIRI BASHUNGWA



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai), akisalimiana na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la TSC, Ndg. Francis Gwankisa alipowasili kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

Utumishi wa Walimu (TSC) pamoja na wadau wote wa Sekta ya Elimu kuitumia vema Kalenda ya Utekelezaji wa Mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari hususani katika utoaji wa tuzo au motisha kwa walimu hapa nchini.

"Pia nimesikia kutakuwa na tukio la kutoa mkono wa pongezi kwa Wastaafu wa Tume. Nawapongeza sana kwa kuwa na utaratibu huu, naomba uendelezwe, uboreshwe, na kudumishwa." Alisema waziri Bashungwa

Nae Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba, alimpongeza kwa dhati Mhe. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyojali Sekta ya Elimu huku akitekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 Na.80 inayolenga: "Kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi."

Vilevile, Mwenyekiti huyo aliipongeza Serikali kwa jitihada za kupambana na janga la ugonjwa wa COVID/ UVIKO-19 na kuweka bayana kuwa TSC inaendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Serikali na Wataalamu wa Afya nchini katika kupambana na janga hili huku akitilia mkazo kwa watumishi na wadau wa Tume kuchukua tahadhari zote dhidi ya janga hilo katika vikao vyote vya Tume ikiwa ni pamoja na kuchanja. "Rai yangu kwenu ambao hamjachanja, mkachanje." Aliyasema



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), akifurahia jambo na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Christina Happe (aliyeshikamanisha mikono yake) kabla ya kupiga picha ya pamoja na meza kuu baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

# PROF. KOMBA: NI JUKUMU LA WALIMU KUFUNDISHA WANAFUNZI MAADILI

**Na. Mwandishi wetu - Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetoa rai kwa walimu nchini kuzingatia maadili katika utumishi wao kwani kazi ya ualimu bila maadili haijakamilika.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba ameyasema hayo hivi karibuni jijini Dodoma alipozungumza na Waandishi wa Habari juu ya maadili ya kazi ya Ualimu.

Prof. Komba amesema kuwa elimu kwa ujumla wake imejikita katika maadili hivyo, bila maadili hakuna elimu kwani inawezekana kwenda shule hadi elimu ya juu lakini kama mtu hana maadili atakuwa amesoma lakini hajaelimika.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba akizungumza na Waandishi wa Habari (hawapo pichani) hivi karibuni jijini Dodoma kuhusu maadili ya kazi ya Ualimu.*

Alifafanua kuwa kwa kiasi kikubwa walimu wamejikita zaidi katika kuwalea watoto kitaaluma lakini malezi ya kiroho yamesahaulika kitu ambacho kinasababisha kuwepo kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii.

"Tunaona kwamba kwenye elimu yetu, walimu wanasoma vyuoni lakini hatuoni matunda mazuri hasa inapokuja suala la kuwalea watoto kiroho. Tunataka mwanafunzi anapopita kwenye mikono ya mwalimu asibubiri hadi shehe au mchungaji amfundishe ndio awe bora kimaadili, siyo lazima aende kanisani au msikitini kujua kipi ni kizuri na kipi ni kibaya," alisema Prof. Komba.

Aliongeza kuwa kwa kutumia mitaala iliyopo sasa, walimu bado wanaweza kuwabadilisha wanafunzi kiroho na kitaaluma ili wawe raia wema wanaoweza



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba akizungumza na Waandishi wa Habari hivi karibuni jijini Dodoma kuhusu maadili ya kazi ya Ualimu. Kushoto (aliyevaa barakoa) ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Mbena Nkwama.*

# PROF. KOMBA: NI JUKUMU LA WALIMU KUFUNDISHA WANAFUNZI MAADILI

kuleta maendeleo chanya katika Taifa.

"Elimu inaenda sambamba na maadili, tunachoona kinachoendelea madarasani, Walimu wetu wengi wanajikita zaidi katika kutoa maarifa kulingana na somo analofundisha lakini suala la maadili wamewaachia viongozi na walimu wenye vipindi vya dini, hii sio sawa", alisema Prof. Komba.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa, "mwanafunzi akielimika katika nyanja moja tu ya taaluma bado haitoshi. Lengo letu ni kuona kadiri mwanafunzi anavyokuwa na maendeleo katika taaluma yake, tuone pia maendeleo chanya katika tabia na maadili kwa ujumla. Mwanafunzi anayebadilika katika nyanja moja tu ya kitaaluma anakuwa bado hajakamilika," alisema.

Prof. Komba amefafanua makosa mazito yaliyokithiri kwa Walimu ikiwemo utoro, kughushi vyeti, uhusiano wa kimapenzi, ukaidi na ulevi ambapo alisema kosa la utoro linashika nafasi ya kwanza katika makosa yote yaliyotendwa na walimu.

Amesisitiza kuwa, adhabu zote zinazotolewa kwa Walimu zinaendana na Kanuni na Taratibu za Tume na kwamba Tume hiyo inajitahidi kutenda haki hivyo, kwa wale ambao hawaridhiki na maamuzi wanaruhusiwa kukata rufaa kwa Kamati ya Nidhamu ya Wilaya, Tume pamoja na kukata rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, Prof. Komba amemshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kibali cha kuwapandisha madaraja walimu 126,346 pamoja na kurekebisha mishahara yao kwa wakati.

Vile vile amewashukuru Walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutoa elimu na kusimamia miradi mbalimbali ya sekta ya elimu kwani pamoja na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo bado viwango vya ufaulu vinaongezeka.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba akizungumza na Waandishi wa Habari hivi karibuni jijini Dodoma kuhusu maadili ya kazi ya Ualimu.*

# SHILINGI MILIONI 31 ZABORESHA MAZINGIRA YA OFISI YA TSC - NJOMBE, INAYOHUDUMIA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE, MJI MAKAMBAKO, NA WILAYA NJOMBE

**Na. Mwandishi Wetu – Njombe**

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Njombe, Mkoani Njombe inayohudumia Halmashauri tatu za Mji Njombe, Mji Makambako, na Wilaya Njombe; inajivunia ukarabati wa jengo la ofisi hiyo uliogharimu jumla ya shilingi 31 milioni zilizotolewa na TSC Makao Makuu, Dodoma ili kuboresha na kuimarisha mazingira ya utoaji huduma kwa walimu wilayani humo ikiwa ni mwendelezo wa uimarishaji miundombinu ya utoaji huduma katika ofisi za TSC wilayani hapa nchini.

Hiyo lilibainika hivi karibuni wakati wa mazungumzo ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara zake za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya na Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Njombe, Ndg. Christopher Henjewele, ikiwa ni mwendelezo wa ziara hizo za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya nchini ili kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC.

"Tunaishukuru Tume Makao Makuu kwa maamuzi ya kutenga na kutupatia jumla ya shilingi milioni 31 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi ambapo sasa umekamilika na tumehamia likiwa limeunganishwa na huduma ya maji na umeme kwa gharama za TSC ambapo awali tulipewa milioni 13 na kumalizia milioni 18 zilizokamilisha ukarabati. Hivyo kwasasa mazingira ya ofisi katika utoaji huduma yameboreka sana hali inayopelekea ari zaidi ya kazi." Alisema Ndg. Henjewele



*Kaimu Katibu Msaidizi) Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Njombe Njombe, Christopher Henjewele akiwa ofisini kwake.*

KKM Henjewele alisema walimu wanaijua vema TSC na Majukumu yake, wanatambua taratibu za kazi, na katika kuimarisha hali ya nidhamu za walimu ambayo kwasasa niya wastani, ofisi yake imekua ikiwatembelea walimu katika vituo vyao vya kazi na kukumbushana misingi na maadili ya ualimu ikiwa ni pamoja na Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Aidha, alisema kwa halmashauri zote tatu zinazohudumiwa na Ofisi ya TSC wilayani Njombe katika kipindi cha mwaka 2018/19 walipokea jumla ya mashauri 17, mwaka 2019/20 walipokea jumla ya mashauri 19, mwaka 2020/21 walipokea jumla ya mashauri 11, na mpaka kufikia Desemba, 2021 ambayo ni nusu mwaka ya mwaka 2021/22 jumla ya mashauri matatu yamepokelewa hii ikiwa ni ishara ya kupungua kwa idadi ya mashauri na kuimarika kwa hali ya nidhamu na uzingatiaji wa maadili.

KKM Henjewele aliongeza kuwa sehemu kubwa ya mashauri ya nidhamu kwa walimu yanatokana na ulevi, ukaidi kwa mamlaka ajira na zile zinazowasimamia, matusi, utoro kazini, kutotimiza majukumu yao

# SHILINGI MILIONI 31 ZABORESHA MAZINGIRA YA OFISI YA TSC - NJOMBE, INAYOHUDUMIA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE, MJI MAKAMBAKO, NA WILAYA NJOMBE

kwa mujibu wa mikataba ya ajira, na kwa uchache sana mahusiano ya mapenzi na wanafunzi.

Pamoja na hayo alisema walimu waliotimiza wajibu wao na kustahili kupandishwa madaraja walipandishwa; ambapo kati ya jumla ya walimu 1,430 waliopandishwa; 598 (331 Msingi na 267 Sekondari) walitoka Halmashauri ya Mji Njombe, 403 (183 Msingi na 220 Sekondari) walitoka Halmashauri ya Wilaya Njombe, na 429 (170 Msingi na 259 Sekondari) walitoka Halmashauri ya Mji Makambako, kutokana na ikama ya 3,021 (Msingi 1,308 na 1,713 Sekondari) kwa Halmashauri ya Mji Njombe, ikama ya 1,776 (Msingi 789 na 987 Sekondari) kwa Halmashauri ya Wilaya Njombe, na ikama ya 1,501 (Msingi 689 na 812 Sekondari) kwa Halmashauri ya Mji Makambako.

Mafanikio hayo alitoa shukrani kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa ushirikiano wao mzuri na mkubwa kuiwezesha kiuchumi na usafiri pale inapolazimu nje ya uwezeshaji wa ndani wa TSC ili kufikia malengo ya utoaji huduma bora kwa walimu wilayani na kuondoa malalamiko.

Ofisi ya TSC Wilayani Njombe, Mkoani Njombe inahudumia jumla ya Halmashauri tatu ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Halmashauri ya Mji wa Njombe na Halmashauri ya Mji wa Makambako zikiwa na jumla ya shule 201 ambazo kati yake Shule za Msingi ni 166 na Sekondari 35 zikihudumiwa na jumla ya Walimu 3,043 ambao kati yao; Walimu 1,576 wanafundisha Shule za Msingi huku Walimu 1,467 wakiwa wanafundisha Shule za Sekondari.










*Mwonekano wa Jengo la Ofisi ya TSC Wilaya ya Njombe baada ya kufanyiwa ukarabati.*

# WAZIRI BASHUNGWA ANAVYOSIKITISHWA NA WALIMU WATORO

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba amesema kuwa utoaji wa mafunzo ni moja ya vipaumbele vya TSC katika kuhakikisha Watumishi wa Tume hiyo, Kamati za Wilaya pamoja na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanatekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi.

Profesa Komba ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alieleza kuwa TSC iliamua kutoa mafunzo kwa kamati za Wilaya baada ya kugundua kuwa kuna udhaifu katika kutoa haki kwa walimu hususan katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na alieleza kuwa udhaifu huo unasababishwa na Wajumbe wa Kamati hizo kutokuwa na uelewa wakutosha katika sheria.

"Tumejikita katika kutoa mafunzo kwa kamati za TSC Wilaya ili kuwaongezea ujuzi wa kutenda haki hususan wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu kwani tumegundua kuwa kuna ukiukwaji mwingi wa taratibu unaofanywa na kamati hizi kutokana na kutokujua sheria na kanuni zake," alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema suala la mafunzunzo sio tu kwamba ni muhimu Kamati za Wilaya peke yake lakini pia kwa tume hiyo inaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake hususan katika eneo la utafiti ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi.

"Hatulengi kutoa mafunzo kwa kamati za Wilaya tu, hapana! Tunalenga pia kuwajengea uwezo watumishi wetu kwani kama mnavyofahamu moja ya majukumu ya TSC kwa mujibu wa sheria ni kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya masuala ya elimu na walimu. Ili tuweze kumshauri ni lazima tufanye tafiti, ndiyo maana tunaona kuna umuhimu mkubwa kuwajengea uwezo watumishi wetu ili waweze kumudu masualala ya tafiti," alieleza.

Kiongozi huyo alikwenda mbali zaidi na kueleza kuwa TSC pia inajipanga kuona namna inavyoweza kutoa mafunzo kwa walimu ili waweze kuetekeleza majukumu yao ipasavyo hususan katika kuwalea wanafunzi kiroho.

Alifafanua kuwa kwa kiasi kikubwa walimu wamejikita zaidi katika kuwalea watoto kitaaluma lakini malezi ya kiroho yamesahaulika kwa kitu ambacho kinasababisha kuwepo kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii.

"Tunaona kwamba kwenye elimu yetu, walimu wanasoma vyuoni lakini hatuoni matunda mazuri hasa inapokuja suala la kuwalea watoto kiroho. Tunataka



*Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai nyekundu), pamoja na meza kuu katika picha ya pamoja na Wastaafu 15 wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mara baada ya kufanya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*

# WAZIRI BASHUNGWA ANAVYOSIKITISHWA NA WALIMU WATORO

mwanafunzi anapopita kwenye mikono ya mwalimu asibubiri hadi shehe au mchungaji amfundishe ndio awe bora kimaadili, siyo lazima aende kanisani au msikitini kujua kipi ni kizuri na kipi ni kibaya," alisema Prof. Komba.

Aliendelea kusema kuwa kwa kutumia mitaala iliyopo sasa, walimu bado wanaweza kuwabadilisha wanafunzi kiroho na wakawa raia wema wenye maadili yanayohitajika katika jamii badala ya kujikita katika kuinua taaluma za wanafunzi peke yake.

"Mwanafunzi akibadilika katika nyanja moja tu ya taaluma bado haitoshi. Lengo letu ni kuona kadiri mwanafunzi anavyokuwa na maendeleo katika taaluma yake, tuone pia anakuwa na maendeleo chanya katika tabia na maadili kwa ujumla. Mwanafunzi anayebadilika katika nyanja moja tu ya taaluma anakuwa bado hajakamilika," alisema.





*Sehemu ya Menejimenti ya Tume na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiimba wimbo wa mshikamano katika mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyazi – TSC, Mwl. Paulina Nkwama (katikati), pamoja na Katibu wa Baraza hilo Ndg. Lawrence Chankan (kushoto kwake) na Katibu Msaidizi Ndg. Neema Lemunge (kulia kwake), wakiimba wimbo wa mshikamano katika mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, Ndg. Evodia Pangani akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha nusu mwaka Julai – Desemba, 2021 katika Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*



*Afisa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini Mkuu, Ndg. Eliah Malaki akiwasilisha Makisio ya Bajeti ya TSC kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 katika Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*



*Katibu wa Kikosi Kazi cha Uratibu wa kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Saccos) na Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Ndg. Nuhu Mlekwa, akiwasilisha Rasimu ya Katiba ya SACCOS ya TSC katika Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*



*Mkurugenzi Msaidizi – Rasilimali Watu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Ndg. Apsa Othman, akiwasilisha majina ya Wastaafu 15 waliopewa Mkono wa Pongezi na kheri ya kustaafu Utumishi wa Umma katika Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyazi – TSC, Mwl. Paulina Nkwama (katikati), pamoja na Katibu wa Baraza hilo Ndg. Lawrence Chankan (kushoto kwake) na Katibu Msaidizi Ndg. Neema Lemunge (kulia kwake), wakinukuu hoja za wajumbe katika mkutano wa baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 19, 2022.*









*Baadhi ya Wastaafu 15 wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwasalimu Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume (hawapo pichani) uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Ndg. Moses Chitama, akiwasilisha Majibu ya Menejimenti kuhusiana na hoja zilizowasilishwa na Watumishi kupitia wajumbe wa Baraza kwa Majadiliano ya pamoja katika Mkutano wa Baraza la Wafanyazi wa Tume hiyo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Naibu Katibu Mkuu – TUGHE Taifa Ndg. Rugemalira Rutatina, akitoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizowasilishwa na watumishi kupitia Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Katibu Mkuu (OR-TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (aliyesimama), akitoa maelezo ya utangulizi kabla ya kumkaribisha Waziri wa Nchi (OR – TAMISEMI), Mhe. Innocent Bashungwa (mwenye tai), kwa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Mmoja wa Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Afisa Maadili na Nidhamu kutoka Ofisi ya TSC Wilayani Mkuranga, Ndg. Christina Ngalawa, akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wajumbe wa mkutano wa baraza mara baada ya baada ya kufungua mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



*Mmoja wa Wastaafu 15 wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akitoa neno la shukrani kwa Menejimenti na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume (hawapo pichani).*



*Mtoa Mada ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mafao kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Ndg. Ramadhan Soshola, akiwasilisha mada hiyo kwa Menejimenti, Wajumbe wa Baraza, na Wastaafu wa Tume ya Utumishi wa Walimu TSC (hawapo pichani) katika mkutano huo wa baraza uliofanyika katika Ukumbi wa 'JK Convention' jijini Dodoma, Januari 20, 2022.*



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***